

HATI YA MAUZIANO YA SHAMBA

Hati ya mauziano ya shamba kati ya Bwana MUSSA PAUL ambaye atatambulika kama Muuzaji yeye na Warithi wake kwa upande mmoja na Bwana GEORGE ISUKANIJA MPEJIWA ambaye atatambulika kama mnunuzi yeye na Warithi wake kwa upande mwingine.

Mimi MUSSA PAUL nikiwa na akili timamu na Kwa hiari yangu nimemuuzia ndugu GEORGE ISUKANIJA MPEJIWA(G1 MINING LTD) eneo lote la Ardhi(Shamba) yangu lenye jumla ya EKARI 10

Linalopakana na G1 MINING LTD Upande wa Mashariki BANAFI NZELA
Upande wa Kusini DEUS GERVAE Upande wa Magharibi

MATTAYO JOSEPH na MARGRETH NGOMBI Upande wa Kaskazini, Leo tarehe 06/12/2019 kwa jumla ya malipo ya Tsh 8,000,000/=(Million Nane (shilingi za Kitanzania)).

Kwa mauziano haya, Mmiliki mpya wa eneo lote hilo kuanzia leo(06/12/2019) ni ndugu GEORGE ISUKANIJA MPEJIWA, Kwa makubaliano yafuatayo na mmiliki wa zamani ndugu MUSSA PAUL;-

- i) Kwamba, mazao yaliyolimwa/yaliyopo shambani yataachwa na mmiliki mpya kwaajiri ya kuvunwa msimu huu na mmiliki wa zamani.
- ii) Kwamba, mmiliki mpya hatahusika na fidia ya aina yoyote juu ya aidha madhara ya maji ya mvua au yanayotoka kwenye mabwawa ya kutunzia maji yasiyo ya kemikali.
- iii) Kwamba, hakutakuwa na malipo mengine yoyote kuhusu jambo lolote juu ya Shamba kwa mmiliki wa Zamani toka kwa mmiliki mpya kuhusu mazao yaliyo shambani, hii ikihusisha na kifungu namba (ii) hapo juu.

- iv) Kwamba, sehemu ya shamba ambayo haitotumika/ haikutumika kwa kilimo na mmiliki wa zamani, mmiliki mpya anaweza kuitumia apendavyo bila kuathiri mazao yaliyolimwa na mmiliki wa zamani.
- v) Kwamba, Makubaliano haya yatakoma tu mara baada ya kamati ya Ardhi kuandikisha makubaliano mapya ya mauziano ambapo kifungu i), ii), iii) na iv) havitabatilishwa.
- vi) Kwamba, Makubaliano haya yamefanyika wakati kamati ya Ardhi ya kijiji ikisubiriwa kuapishwa na kuanza kazi na pindi ikianza kazi, wahusika wataenda kwenye balaza ili kupitisha makubaliano haya. Gharama zote za malipo ya ofisi/kamati ya Ardhi za uandikishaji nyaraka za kisheria kuhusiana na mauziano haya zitasimamiwa na mmiliki mpya.
- vii) Kwamba, baada ya kuvuna mazao ya msimu huu, Mmiliki wa zamani atavuna pia milingoti ya katani na miti ya kupanda (Miboyo) wakati wa kiangazi na atamuachia miti yote ya matunda bila kuiathiri pamoja na Miti ya Asili iliyopo

JINA LA MUUZAJI	SAHIHI/DOLE	NA. YA SIMU	TAREHE
<u>MWA PAOLO</u>	<u>MWA</u>	<u>0759088405</u>	<u>06-12-2019</u>
JINA LA MNUNUZI	SAHIHI/DOLE	NA. YA SIMU	TAREHE
<u>GEORGE MPEJIWA</u>	<u>MS</u>	<u>0753233830</u>	<u>06/12/2019</u>

Makubaliano haya yamefanyika mbele ya ushahidi wa ;

Jina Tarehe	Sahihi/Dole	Na.ya Simu(Muuzaji)	Tarehe
i) <u>JOSEPH MUSA</u>	<u>MS</u>	<u>—</u>	<u>06/12/2019</u>
ii) <u>OSCAR MAKUME</u>	<u>MS</u>	<u>0767609465 (Mnunuzi)</u>	<u>06/12/2019</u>